**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI MBEYA**

**Kumb.Na. HA.145/325/01/01/45** **16 Januari, 2026**

## *TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA*

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa kuzingatia Kanuni ya 111 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 anawatangazia watu wote wenye sifa kuomba kazi ya nafasi ya **Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira**.

### A. SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe raia wa Tanzania.
ii. Awe Mkazi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya.
iii. Awe Mstaafu Serikalini.
iv. Awe hajawahi kushtakiwa kwa kosa lolote la Jinai.
v. Awe na Umri kuanzia miaka 55 hadi 65 (Sitini na tano).
vi. Awe na Elimu ya Form IV au Form VI.
vii. Awe na Taaluma ya kuanzia Stashahada ya Juu/Shahada katika fani ya Sayansi ya Jamii katika Sheria, Utawala au Usimamizi wa Rasilimaliwatu.

### B. MAJUKUMU

i. Kuendesha/kuongoza vikao vya Usaili wa waombaji wa nafasi za kazi.
ii. Kuendesha/kuongoza vikao vya kuwathibitisha kazini watumishi.
iii. Kuongoza/kuendesha vikao vya kupandisha/kuwabadilisha watumishi vyeo.

### C. POSHO

Kazi hii haina Mshahara wa kila mwezi. Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atakuwa analipwa posho kutokana na vikao vitakavyokaliwa na Bodi.

### D. MASHARTI YA JUMLA

i. Mwombaji aambatishe Wasifu wake kwenye barua yake ya maombi.
ii. Mwombaji aambatishe nakala halisi ya vyeti vyake vya elimu na taaluma.
iii. Kila mwombaji aambatishe picha 2 za pasipoti katika maombi yake.
iv. Mwombaji aambatishe barua ya utambulisho toka Serikali ya Mtaa anapoishi.

Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashuari ya Jiji la Mbeya kuanzia tarehe **16/01/2026** na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **23/01/2026** saa 9:30 alasiri

Anwani ya kutuma maombi,

**Mkurugenzi wa Jiji,**
**Halmashauri ya Jiji la Mbeya,**
**S. L. P. 149,**
**MBEYA**

Dkt. Lawrence Kibona
**KAIMU MKURUGENZI WA JIJI**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI
MBEYA

Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, S.L.P 149, 1 Mtaa wa Maktaba, 53182 MBEYA Simu: +255 25 2502372,Nukushi:+255 25 2502488,Barua pepe:cd@mbeyacc.go.tz,Tovuti:www.mbeyacc.go.tz